

## Mtoto Umleavyo...

- Mvulana:** Shikamoo baba.
- Baba:** Marahaba wewe viper?
- Mvulana:** Safi tuu baba.
- Baba:** Huu mpira wa nani? Au mama yako amekununulia mpira mpya?
- Mvulana:** Hapana baba.
- Baba:** Sasa umeutoa wapi?
- Mvulana:** Nimeutoa pale nje niliona hamna mtu anayechezea Nikauchuku
- Baba:** Hebu tuone
- Mvulana:** Baba unafanya mazoezi
- Baba:** Ndiyo unafaa

## Siku ya pili

- Mvulana:** Hodii baba?
- Baba:** Karibu.
- Mvulana:** Shikamoo baba.
- Baba:** Marahaba, hujambo?
- Mvulana:** Sijambo baba.
- Baba:** Kwema huko?
- Mvulana:** Kwema tuu.
- Baba:** Mboma una wasawasi?
- Mvulana:** Wala sina wasiwasi baba.

### (mlio wa simu)

- Baba:** Hiyo nini? Hebu lete tuone?
- Mvulana:** Hamna kitu baba.
- Baba:** Mboma unajishikashika?
- Mvulana:** Hamna baba.
- Baba:** Wewe mtoto siku hizi una simu?
- Mvulana:** Ndiyo baba.
- Baba:** Kasimu! kazuri, umetoa wapi?
- Mvulana:** Nimeokota baba.
- Baba:** Umeokota simu!
- Mvulana:** Ndiyo baba, kasimu kazuri kweli.

- Baba:** Basi hii simu mimi nitakaanayo.
- Mvulana:** Sawa baba.

### **Siku ya tatu**

- Mvulana:** Shikamoo baba,
- Baba:** Marahaba.
- Mvulana:** Pole na kazi baba,
- Baba:** Haya asante.
- Mvulana:** Unajua baba leo nina usafiri.
- Baba:** Na hii umetoa wapi leo?
- Mvulana:** Hii nilipewa na rafiki yangu, rafiki yagu alinunuliwa na baba yake baiskeli nyingine akaamua kunipa hii.
- Baba:** Kwa hiyo ni ya rafiki yako wa zamani akaamua kukupa hii baiskeli
- Mvulana:** Ndiyo baba
- Baba:** Kazuri kweli
- Mvulana:** Ndiyo baba
- Baba:** Sasa mimi naweza kuendeshaendesha maana mimi nimeendesha baiskeli zamani sana kuliko wewe
- Mvulana:** Kazuri kweli! Kanafaa kweli!

### *(Baadaye kidogo)*

- Mzee:** Hodi hapa.
- Baba:** Karibuni.
- Mzee:** Habari za hapa.
- Baba:** Nzuri tuu.
- Mzee:** Mtoto wako ni mwizi ameniibia baiskeli.
- Baba:** Mwanangu siyo mwizi, wala hajaiba kwa mtu. Sipendi mnyanyasa mwanangu.
- Kijana:** Mtoto wako ni mwizi sana.
- Baba:** Hii baiskeli kapewa na rafiki yake wala hajaiba!
- Mzee:** Mtoto umleavyo, ndivyo akuavyo. Huyu mtoto nampeleka polisi leo!
- Mvulana:** Baba naomba nisaidie (huku akilia).

**Baba:** Usijali mwanangu nitakusaidia.  
Mzee basi tukae chini halafu tuyazungumze

**Mzee:** Hamna cha kuzungumza leo! Nampeleka polisi

**Kijana:** Siyo balskeli tuu ameiba kaiba vitu vingi sana

**Mvulana:** Nisaidie baba...

**Baba:** Nitakusaidia tuu.